

القرآن الحكيم

QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

46. Anayefanya mema anajifanyia (mwenyewe) nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu (ya nafsi) yake (vile vile); na Mola wako si dhalimu (hata kidogo) kwa waja (wake).

47. Ujuzi wa kujua Kiama unarudishwa Kwake (tu Mwenyezi Mungu). Na matunda hayatoki katika mafumba yake, (vifuniko vyake), wala mwanamke hachukui mimba wala hazai ila kwa ujuzi wake. Na siku atakayowaita (Mwenyezi Mungu akawaambia): "Wako wapi washirika wangu?" Hapo watasema (hao washirikina): "Twakiri kwako ya kuwa hakuna miongoni mwetu anayeshuhudia (kuwa Wewe una mshirika)."

48. Na wale waliokuwa wakiwaabudu zamani, sasa wamewapotea, na wameyakinisha ya kuwa hawana pa kukimbilia.

49. Mwanaadamu hachoki kuomba dua za kheri, (na Mwenyezi Mungu anampa, na shukrani hana); na inapompata shari, mara hukata tamaa na kuwa na bila tumainio lolote.

50. Na kama tukimuonjesha rehema yetu baada ya dhara iliyomgusa, mara husema: "Haya nayastahiki mimi (mwenyewe; hapana haja ya shukrani), wala sidhani ya kwamba Kiama kitatokea; na kama nikirudishwa kwa Mola wangu (haidhuru); bila shaka nina mema (yangu) kwake." Basi tutawajulisha wale waliokufuru hayo waliyoyatenda na tutawaonjesha adhabu ngumu.

51. Na tunapomneemesha mwanaadamu, hugeuka na kujitenga upande, (hana haja ya kutuabudu); na inapomgusa shari, mara hugeuka akawa ana madua marefu marefu.

52. Sema: "Mwaonaje! Ikiwa (maneno haya) yametoka kwa Mwenyezi Mungu, kisha nyinyi mkayakanusha (si mumepotea hivyo kwani), ni nani aliyepotea zaidi kuliko yule aliye katika upinzani wa mbali (kabisa na haki)?"

53. Tutawaonyesha (ukweli wa) maneno yetu haya katika nchi za mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwa Mola wako kuwa Yeye ni mjuzi wa kila kitu?

54. Tahadharini! Wamo katika shaka katika kukutana na Mola wao! Hakika Yeye (Mola wao) amekizunguka, (anakijua vyema) kila kitu.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا
وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِلْعَبِيدِ ٥٦

إِلَيْهِ يُرْجَىٰ عِلْمُ السَّاعَةِ وَمَا تَخْرُجُ مِنْ ثَمَرَاتٍ
مِّنْ أَكْثَامِهَا وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنْثَىٰ وَلَا تَضْمُ إِلَّا
بِعِلْمِهِ ۚ وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ أَيْنَ شُرَكَائِيَ ۖ قَالُوا
أَذْنَبْنَا قَسَمًا مِّنْ شَيْءٍ ۚ

الْقُرْآنُ الْمَجِيدُ

وَصَلَّىٰ عَنْهُمْ مَّا كَانُوا يَدْعُونَ مِن قَبْلُ
وَوَدَّ أَن يُسْأَلَ لَّهُم مِّنْ مَّحِيصٍ ٥٧

لَا يَسْأَلُ إِلَّا نَاسًا مِّنْ دُعَاءِ الْخَيْرِ ۚ وَإِنَّ مَصْرَهُ
الشُّرَكَايَا قَتَلُوا ٥٨

وَلَكِنْ أَذَقْنَاهُ رَحْمَةً مِّنَّا مِن بَعْدِ صَرَائِرِ مَا
كَفَرُوا ۚ هَذَا لِيَوْمَ أَطْلُقُ السَّاعَةَ قَائِمَةً ۚ
وَلَكِنْ تُرْجَعُ إِلَىٰ رَبِّي إِنْ لِّيَ عِنْدَهُ لَلْحُسْبَىٰ ۚ
فَلَنُكَلِّمَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنَّا عَمَلُهُمْ وَلَنُنْذِرَنَّهُمْ
مِّنْ عَذَابٍ غَلِيظٍ ٥٩

وَأَذَّا أَلْعَمْنَا عَلَىٰ الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَأٰ بِجَانِبِهِ
وَأَذَّا مَصْرَهُ الشُّرَكَاءُ فَذُو دُعَاءِ عَرِيضٍ ٦٠


قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ مِنَ عِنْدِ اللَّهِ ثَمَرٌ
كَفَرْتُمْ بِهِ مِنْ أَصْلٍ مِّنْهُ هُوَ فِي شِقَاقٍ
بَعِيدٍ ٦١

سَنُرِيهِمْ آيَاتِنَا فِي الْأَقَا فِي أَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ
يَتَّبِعِينَ لَّهُمُ اللَّهُ الْحَقُّ ۚ أَوَلَمْ يَكُفْ بِرَبِّكَ أَنَّ اللَّهَ
عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ٦٢

أَلَا إِنَّهُمْ فِي مَرِيضَةٍ مِّنْ لِّقَاءِ رَبِّهِمْ ۚ أَلَا إِنَّهُ
بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطٌ ٦٣

٦٣

53. Tumebainisha mara nyingi baadhi ya hayo yaliyosemwa katika Qurani ambayo hayakuwa yakidhaniwa kuwa yataitakidiwa seuze kuonekana kutokea. Sasa yametokea na ulmwengu mzima yameonekana.



Ina Aya 53

SURATUSH SHUURA

Ina Makara 5

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Haa Mym.
2. Ayn Syn Qaf.
3. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima anavyokuletea Wahyi (anavyokufunulia) wewe na (alivyowafunulia) wale waliokutangulia.

4. Ni Vyake (vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Yeye ndiye aliye juu, Mkuu.

5. Zinakaribia mbingu kupasuka juu yao (kwa kumuogopa Mola wake). Na Malaika wanamtukuza Mola wao na kumshukuru na kuwaomba msamaha walio katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha (na) Mwenye huruma.

6. Na wale walioshika waungu wengine badala yake (Mwenyezi Mungu). Mwenyezi Mungu anawawekea kila wayafanyayo, na wewe siye unayehifadhi amali zao.

7. Na namna hivi tumekufunulia Qurani kwa Kiarabu ili uwaonye watu wa Makka na walio (katika nchi zilizo) pembeni mwake. (Nao ni ulimwengu mzima kwani Makka iko katikati ya ulimwengu). Na uwaonye siku ya mkutano; Siku isiyo na shaka (kuwa itakuja). Kundi moja litakuwa Peponi na kundi jingine Motoni.

8. Na Mwenyezi Mungu angalipenda angewafanya wote kundi moja, lakini anamuingiza

خَم ①
عَسَق ②
كَذَلِكَ يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِنْ
قَبْلِكَ ۚ اللَّهُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ③

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَلِيُّ
الْعَظِيمُ ④

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْ فَوْقِهِنَّ
وَالْمَلَائِكَةُ يَسْجُدُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ
وَيَسْتَغْفِرُونَ لِمَنْ فِي الْأَرْضِ ۚ إِلَّا لِمَنْ
هُوَ الْعَفْوَ الرَّحِيمُ ⑤

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ اللَّهُ
حَفِيفٌ عَلَيْهِمْ ۚ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ⑥

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِتُنْذِرَ
أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا ۚ وَتُنْذِرَ يَوْمَ الْجُمُعِ
لَا رَيْبَ فِيهِ ۚ فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ⑦

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَهُمْ أُمَّةً ۚ وَاحِدَةً ۚ وَلَكِنْ

3. Hii ndiyo haki aliyosema Mwenyezi Mungu katika Qurani yote na akasema Mtume katika Hadithi zake zote kuwa Utume wa haki ni huo aliopewa yeye na waliopewa Mitume wa haki waliokuwa kabla yake, (Minqablika). Hakuna katika Qurani Minbaadika, (watakaopewa Utume baada yake). Na haya tumeyabainisha mahala pengi. Na pa mwisho ni katika maelezo ya Aya ya 40 ya Suratul Ahzab.

7. Tafsiri ya kweli katika hizo tafsiri tatu walizozitilia Aya hii waliyoifanya ya 8, ni ile ya (2) tu.

8. Tumebainisha mara nyingi kuwa maelezo ya Aya hizi zilizo Mutlaq hufahamika katika zile Muqayyad,

katika rehema yake amtakaye (kwa kuwa amefuata amri zake). Na madhalimu hawana mlinzi wala msaidizi.

9. Oh! Wao wameshika waungu wengine badala yake! Lakini mlinzi hasa ni Mwenyezi Mungu, na Yeye ndiye atakayewahisha waliokufa Naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

10. Na mkihitalifiana katika jambo lolote (rejeleeni kitabu cha Mwenyezi Mungu na Hadhithi za Mtume kwani) hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Huyu Mwenyezi Mungu ndiye Mola wangu ninayemtegemea, na Kwake ninarejea.

11. (Yeye ndiye) Muumba wa mbingu na ardhi. Amekuumbieni wake (zenu) katika jinsi yenu; na wanyama nao (akawaumbia) wake (zao katika jinsi moja na wao); anakuzidisheni kwa namna hii (ya kuchanganyika dume na jike). Hakuna chochote mfano Wake; naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

12. Funguo za mbingu na ardhi ziko katika kabdhi Yake. Humfungulia riziki amtakaye na humdhikishia (amtakaye kwa maslahi ya huyo kiumbe). Bila shaka Yeye ndiye ajuaye kila kitu.

13. Amekupeni Sharia ya dini ile ile aliyomuusia Nuhu na tuliyokufunulia wewe na tuliyowausia Ibrahimu na Musa na Isa, kwamba simamisheni dini wala msifarikiane kwayo, (kwa ajili ya dini); ni ngumu kwa wenye kushirikisha (dini hii) unayowaitia; Mwenyezi Mungu humchagua Kwake amtakaye na humuongoza Kwake aelekeaye (Kwake).

14. Na hawakutengana (wakawa mapote mbali mbali yasiyopatana) ila baada ya kuwajia ilimu. (Na yote haya) kwa sababu ya kuhusudiana baina yao; na kama isingalikuwa kauli iliyotangulia kutoka kwa Mola wako (ya kuwa kuadhibiwa ni) mpaka muda wake uliowekwa, hukumu ingalitolewa (sasa hivi baina yao). Na kwa yakini wale waliorithishwa Kitabu baada yao (hao waliopita), wanakitilia shaka inayowahangaisha.

(zilizobainisha shuruti). Basi Mwenyezi Mungu anawatia katika rehema zake wale wanaostahiki hizo rehema, kama alivyobainisha mahala pengi; na pamoja katika humo ni Aya ya 156 ya *Suratul Aaraf*. Na kama alivyobainisha hapa kuwa wanaodhulumu, (ikiwa nafsi zao au wengineo) hawapati rehema yake.

10. Haya tunaambiwa kila siku, na kusikia hakuna — kuwa ikitokea khitilafu baina ya watu kuwa hili linafaa au halifai, itazamwe Mwenyewe Mungu amesema nini au Mtume amesema nini. Lifuatwe hilo la Mungu kama liko, au la Mtume ikiwa hapana la Mungu. Ikiwa yote hapana — hata kwa ishara tu — litazamwe lipi lililoelekea zaidi. Yakiwa yote sawa sawa; basi wanaotaka wafuate hili na wanaotaka wafuate lile bila kutiliana mifundo wala mashindano.

يَدْخُلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ وَالظَّالِمُونَ مَا لَهُمْ مِنْ وَجِيلٍ ۚ وَلَا نَصِيرٍ ۝

أَمِ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۚ قَالَ اللَّهُ هُوَ الْوَلِيُّ ۖ وَهُوَ يُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ۝

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِنْ شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ ذَلِكُمُ اللَّهُ رَبِّي عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ۝

فَاطِرُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا ۚ وَمِنَ الْأَنْعَامِ أَزْوَاجًا ۚ يَذَرُوكُمْ فِيهِ وَلَيَسَ كَيْثَلُهُ شَيْءٌ ۚ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ۝

لَهُ مَقَالِيدُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۚ إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ۝

شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ ۚ كَبُرَ عَلَى الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ ۚ اللَّهُ يَجْتَبِي إِلَيْهِ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ يُنِيبُ ۝

وَمَا تَفَرَّقُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَعِيًّا ۚ بَيْنَهُمْ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى لَفُضَّ بَيْنَهُمْ ۚ وَالَّذِينَ آوَرْتُوا الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِهِمْ لَنْ نَكْفِيَكَ مِنْهُ مَرْبٍ ۝

15. Waite kwenda kufanya haya, na mwenyewe utengenee (unyoke) kama ulivyoamrisha, wala usifuatue matamania yao; na useme: "Naamini vitabu alivyoteremsha Mwenyezi Mungu; na nimeamrisha nifanye uadilifu baina yenu; Mwenyezi Mungu ndiye Mola wetu na (pia) ni Mola wenu; vitendo vyetu ni kwa ajili yetu, na vitendo vyenu ni kwa ajili yenu (wenyewe); hakuna ugomvi baina yetu na nyiye; Mwenyezi Mungu atatukusanya pamoja, na marejeo ni Kwake."

16. Na wale wanaohojiana juu ya (dini ya) Mwenyezi Mungu baada ya kukubaliwa, hoja zao ni batili mbele ya Mola wao, na juu yao iko ghadhabu na itakuwa kwao adhabu kali (siku ya Kiama).

17. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeteremsha Kitabu (hiki) kwa (kubainisha) haki na mizani. Na ni nini kitakachokujulisha ya kwamba labda Kiama kimekaribia?

18. Wasioamini, (kwa stihzai yao) hukuomba (Kiama) kifike upesi; lakini wanaoamini wanakiogopa na wanatambua kwamba (kuja kwake) ni haki, (kitatokea tu). Kwa hakika hao wanaobishana katika (habari ya) Kiama wamo katika upotofu (upotevu) wa mbali kabisa.

19. Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa (waja) Wake, anampa riziki amtakaye; naye ni Mwenye nguvu, Mbora (au) Mwenye kushinda.

20. Mwenye kutaka jaza ya Akhera tutamzidishia katika jaza yake hiyo; na anayetaka jaza ya dunia tutampa, lakini Akhera hatakuwa na sehemu yo yote ya kheri.

21. Oh! Wana washirika (wa Mwenyezi Mungu) waliowawekea dini asiyoitolea Mwenyezi Mungu ruhusa (yake)? Na kama lisingalikuwako neno la (kuwa iko siku ya) kupambanua hukumu (huko Kiama), basi hukumu ingalikakwa baina yao (sasa hivi); na kwa yakini itakuwa kwa madhalimu adhabu iumizayo.

22. Utawaona (siku ya Kiama) madhalimu wanavyotetemeka kwa sababu ya yale waliyoyachuma; nayo yatawatokea tu; na wale walioamini na kutenda wema watakuwamo katika mabustani ya Peponi; watapata watakatayoyataka kwa Mola wao. Hiyo ndiyo fadhila kubwa.

قَدْ لَكُمْ فَادْرُ : وَاسْتَقِمَّ كَمَا أُمِرْتُمْ وَلَا
تَتَّبِعُوا أَهْوَاءَهُمْ وَقُلْ أَمَّا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ
كِتَابٍ : وَأُمِرْتُ لِأَعْدِلَ بَيْنَكُمْ اللَّهُ رَبُّنَا
وَرَبُّكُمْ لَنَا أَعْمَالُنَا وَلَكُمْ أَعْمَالُكُمْ
لَا حِجَّةَ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ اللَّهُ يَجْمَعُ بَيْنَنَا
وَالْيَوْمِ الْمَعْيُورِ ⑤

وَالَّذِينَ يُحَاجُّونَ فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا
اسْتُجِيبَ لَهُمْ حُجَّتُهُمْ دَاحِضَةً عِنْدَ رَبِّهِمْ
وَعَلَيْهِمْ عَذَابٌ وَعَلَيْهِمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ⑥
اللَّهُ الَّذِي أَنْزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَالْمِيزَانَ
وَمَا يَدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ قَرِيبٌ ⑦

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا
وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا
الْحَقُّ ⑧ أَلَا إِنَّ الَّذِينَ يُمَارُونَ فِي السَّاعَةِ
لَفِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ⑨

اللَّهُ لَطِيفٌ بِعِبَادِهِ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ :
وَهُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ ⑩

مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي
حَرْثِهِ : وَمَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ
مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ ⑪
أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ
يَأْذَنْ بِهِ اللَّهُ وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَفُضِلَ
بَيْنَهُمْ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ⑫

تَرَى الظَّالِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا كَسَبُوا وَهُمْ وَاقِعٌ
بِهِمْ : وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
فِي رَوْضَاتِ الْجَنَّاتِ لَهُمْ مَا يَشَاءُونَ
عِنْدَ رَبِّهِمْ ذَلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ ⑬

23. Hii ndiyo habari nzuri ambayo Mwenyezi Mungu anawaambia waja wake walioamini na kufanya vitendo vizuri. Sema: Kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu). Na anayefanya wema tutamzidishia wema; kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa shukrani.

24. Ndio wanasema: "Amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo?" Kama Mwenyezi Mungu akitaka atapiga muhuri moyoni mwako (usiweze kusema lolote). Na Mwenyezi Mungu anaifuta batili na anathubutisha ukweli kwa maneno Yake. Bila shaka Yeye anayajua yaliyomo vifuani (mwa viumbe Vyake, seuze ya dhahiri).

25. Naye ndiye anayepokea toba za watu Wake, na anasamehe makosa, na anayajua yote mnayoyatenda

26. Na anawajibu wanaoamini na kutenda mema, na anawazidishia fadhila Zake. Na makafiri watakuwa na adhabu kali.

27. Na kama Mwenyezi Mungu angetoa riziki nyingi kuwapa waja Wake, bila shaka wanalitakabari (wangeliasi zaidi) katika ardhi, lakini

ذَٰلِكَ الَّذِي يُبَيِّنُ اللَّهُ عِبَادَهُ الَّذِينَ أَمْنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ وَمَن يَقْتَرِفْ حَسَنَةً نَّزِدْ لَهُ فِيهَا حُسْنًا إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٢٣﴾

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا، فَإِنْ يَشَأِ اللَّهُ يَخْتِمْ عَلَىٰ قَلْبِكَ، وَيَمَسُّهُ اللَّهُ الْبَاطِلَ وَيُحِقُّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٢٤﴾

وَهُوَ الَّذِي يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ وَيَعْفُو عَنِ السَّيِّئَاتِ وَيَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٢٥﴾ وَيَسْتَجِيبُ الَّذِينَ أَمْنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَيَزِيدُهُم مِّن فَضْلِهِ، وَالْكَافِرُونَ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ﴿٢٦﴾

وَلَوْ بَسَطَ اللَّهُ الرِّزْقَ لِعِبَادِهِ لَبَغَوْا فِي الْأَرْضِ

23. Hii ndiyo tafsiri nzuri kuliko zote na unyukubaliwa na wanavyuoni wengi na inayokubaliana na Aya zilizopita na zitakazokuja. Kadhalika ndiyo tafsiri inayokubaliana na mafundisho ya dini ya Kiislamu. Ziko tafsiri nyengine ambazo hazikubaliani na hayo yote. Na mbaya kuliko zote ni, "Siombi malipo yoyote kwenu ulla kuwapenda jamaa zangu."

Tunasema kuwa tafsiri hii ni dhaifu sana kwa sababu—

(a) Tafsiri hii inaonesha kuwa Mtume Muhammad alitaka Ujira wa namna fulani juu ya kazi yake. Na hili halikubaliani na Aya nyengine zote zilizomo katika Qurani yote. Katika *Suratish Shuaraa* vimetajwa visa vya Mitume kadha wa kadha waliopolekwa kwa Umma mbali mbali; na kila mmoja katika hao akakataa ujira wa namna yoyote. (Soma Aya hizi—109, 127, 145, 164, 180). Na katika Aya za namna hiyo zenye kumukhusu Mtume Muhammad ameamrisha vile vile kukataa ujira wa namna yoyote. (Soma *Surat Yusuf* Aya 104, na *Sura: Tu'r* Aya 40 na *Surat Alqalam* Aya 46 na nyenginezo).

(b) Kuwaamrisha watu wawapende jamaa za Mtume ni kuwaamrisha walipe Ujira mkubwa zaidi kuliko ujira wa mali kwani kumpenda mtu usiyempenda ni taabu zaidi kuliko kumpa kitu.

(c) Tafsiri hii haikubaliani na tabia ya kibinadamu kwani tabia ya kibinadamu ni kumpenda aliyekutenda mema na kumchukia aliyekutenda mabaya. Na iwapo mtu atalazimishwa kuwapenda jamaa wa Mtume wote itamlazimu kuwapenda hata waliomtenda mabaya katika wao; na hilo ni jambo lisilowezekana. Mapenzi ni kitu ambacho mtu hakimiliki, yaani mtu hawezi kuyaweka anapotaka yeye, bali yanakwenda kwa mujibu wa tabia ya kibinadamu. Kwa mfano Waislamu wanaamrisha kufanya usawa baina ya wake, na Mtume mwenyewe alikuwa na jitihadi kubwa ya kufanya usawa baina ya wake zake katika kila kitu; lakini alishindwa kufanya usawa katika mapenzi. Kwa hivyo alikuwa akisema katika dua zake, "Ewe Mwenyezi Mungu! Hiki ndicho kigawanyo changu katika ninalolimiliki, basi nighufiria katika nisilolimiliki (yaani mapenzi)."

Waislamu wote wanaamrisha wapendane, na kupendana maana yake ni kila mmoja ampende mwenzake. Na wakati huo huo wameamrisha wajipambe kwa tabia njema ambazo zinavuta mapenzi ya watu, na kuepukana na tabia ambazo zinawapelekea kuchukiana.

anaiteremsha kwa kipimo akitakacho. Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye habari (zao zote) na Mwenye kuwaona.

28. Naye ndiye anayeteremsha mvua baada ya wao kukata tamaa, na hueneza rehema Yake (kwa mvua hiyo). Naye ndiye Mlinzi anayeshukuriwa.

29. Na katika Ishara Zake (za kuwa yuko) ni huku kuumbwa mbingu na ardhi na hivi vyenye uhai alivyovieneza humo; na Yeye ni Mwenye uweza wa kuvikusanya apendapo.

30. Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu, na (juu ya hivi Mwenyezi Mungu) anasamehe mengi.

31. Na nyinyi hamuwezi kumshinda (Mwenyezi Mungu) hapa katika ardhi, (seuze mbinguni); na hamna mbele ya Mwenyezi Mungu mlinzi wala msaidizi.

32. Na katika Ishara zake (za neema zake juu yenu) ni vyombo (vinavyokwenda na kurejea) baharini vilivyo kama milima (kwa ukubwa wake).

33. Kama akitaka hutuliza upepo, nayo (hayo majahazi) husimama tutwe juu yake; kwa yakini katika haya ziko Ishara kwa kila afanyaye subira sana, na kushukuru sana

34. Au huyaangamiza (akawagharikisha waliomo ndani yake) kwa sababu ya yale waliyoyatenda; na anasamehe mengi.

35. Na watajua (siku ya Kiama) wale wanaojadiliana katika Aya zetu (ya kwamba) hawana mahali pa kukimbilia.

36. Basi vyote hivi mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora na cha kudumu (milele). Watahistahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea Mola wao.

37. Na wale wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo mabaya, na wale ambao wanapokasirika husamehe.

38. Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri Zake) na wakasimamisha Sala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyouwaruzuku.

وَلَكِنْ يُنْزِلُ بِقَدَرٍ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّهُ بِعِبَادِهِ خَبِيرٌ بَصِيرٌ ﴿٢٨﴾

وَهُوَ الَّذِي يُنْزِلُ الْغَيْثَ مِنْ بَعْدِ مَا قَنَطُوا وَيَنْشُرُ رَحْمَتَهُ ۚ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٢٩﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا مِنْ دَابَّةٍ ۚ وَهُوَ عَلَىٰ جَمْعِهِمْ إِذَا يَشَاءُ قَدِيرٌ ﴿٣٠﴾

وَمَا أَصَابَكُمْ مِنْ مُصِيبَةٍ فَمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ ﴿٣١﴾

وَمَا أَتَاكُمْ مِنْ مَعْجَزِينَ فِي الْأَرْضِ ۖ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٣٢﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ الْجَوَارِ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَامِ ﴿٣٣﴾

إِنْ يَشَاءِ يُخْسِفِ الرِّيحَ فَيَظْلِلْنَ رَوَاكِدَ عَلَى ظَهْرِهِ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٣٤﴾

أَوْ يُوقِفَهُنَّ بِمَا كَسَبْنَ وَيَعْفُ عَنْ كَثِيرٍ ﴿٣٥﴾

وَيَعْلَمُ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِنَا مَا لَهُمْ مِنْ مُجِيبٍ ﴿٣٦﴾

فَمَا أَوْتَيْنَاهُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّاءُ الْحَيَوةِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٣٧﴾

وَالَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كِبْرَ الْأَيْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَإِذَا مَا غَضِبُوا هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٣٨﴾

وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ ۚ وَأَمْرُهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٩﴾

36-43. Hizi ni sifa ambazo inampasa kila Mislamu kusifika nazo, ndipo awe Muislamu wa kweli.

38. Wamejitia kutia tamko la Khalifa ili wawatie hao watu wao wanaowaita Makhalifa. Hao ni watu wao si watu wa Waislamu.

39. Na wale ambao jeuri inapowafikia huzitetea nafsi zao.

40. Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na (ubaya) huo; lakini anayesamehe na kusuluhisha ugomvi; ujira wake uko kwa Mwenyezi Mungu; bila shaka Yeye hawapendi madhalimu.

41. Na wale wanaolipiza kisasi baada ya kudhulumiwa, hao hakuna njia ya kulaumiwa.

42. Bali lawama iko juu ya wale wanaodhulumu watu na wakawafanyia jeuri katika ardhi pasipo haki; hao ndio watakaopata adhabu iumizayo.

43. Na anayesubiri na kusamehe (atalipwa wema wake). Bila shaka hilo ni katika mambo makubwa ya kuazimiwa kufanywa (na kila Muislamu).

44. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamwacha kupotea, hana mlinzi baada Yake. Na utawaona madhalimu watakapoiona adhabu wanasema (kwa masikitiko): "Je! Iko njia ya kurudi (ulimwenguni tukafanye mema tupate Pepo)?"

45. Na utawaona wanapelekwa (kwenye Moto); wamekuwa wanyonge kwa dhila, wanatazama (yanayopita) kwa mtazamo wa kificho. Na walioamini watasema: "Kwa hakika wapatao hasara ni wale waliohasirisha nafsi zao na watu wao siku (ya leo hii) ya Kiama." Bila shaka madhalimu watakuwa katika adhabu inayoendelea.

46. Wala hawatakuwa na marafiki wa kuwasaidia mbele ya Mwenyezi Mungu. Na ambaye Mwenyezi Mungu anamuacha kupotea, hana njia yoyote (ya kutengenea).

47. Mwitikieni Mola wenu kabla ya kufika siku isiyoepukika itokayo kwa Mwenyezi Mungu, siku hiyo hamtakuwa na pa kukimbilia wala hamtakuwa na (njia ya) kukataa (mtakayofanyiwa).

وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٣٩﴾

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۚ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾

وَلَكِنْ انْتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَٰئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِنْ سَبِيلٍ ﴿٤١﴾

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۚ أُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

وَلَكِنْ صَبَرُوا وَعَفَوْنَا ۚ ذَٰلِكَ لِمَنْ عَزَمَ الْأُمُورُ ﴿٤٣﴾

وَمَنْ يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ سَبِيلٍ ۚ وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ بَعْدِهِ ۚ وَتَرَى الظَّالِمِينَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ يَقُولُونَ هَلْ لَنَا مَرَدٌّ مِّنْ سَبِيلِ اللَّهِ

وَتَرَاهُمْ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا خَشِيعَتٍ مِّنَ الدَّلِيلِ يَنْظُرُونَ مِّنْ طَرَفٍ خَفِيفٍ ۚ وَقَالَ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ الْآخِرِينَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَآهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۚ أَلَا إِنَّ الظَّالِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّقِيمٍ ﴿٤٤﴾

وَمَا كَانَ لَهُمْ مِّنْ أَوْلِيَاءَ يَنْصُرُونَهُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ ۚ وَمَنْ يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ سَبِيلٍ ۚ

إِسْتَجِيبُوا لِلرَّسُولِ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدٍّ لَهُ ۚ مِّنَ اللَّهِ ۚ مَا لَكُمْ مِّنْ مُّجَلٍّ ۚ يَوْمَئِذٍ تَوَدُّ لَكُمْ مِّنْ تَكْوِينٍ ﴿٤٥﴾

39. Katika Aya hizi kuna sifa mbili, utaona kama kwamba zinapingana. Katika Aya ya 37 imeambiwa wakiudhiwa wanasamehe. Na katika Aya ya 39 hii wanaambiwa wanalipa kisasi. Basi hazipingani. Bali wanaambiwa wapime. Ikionekana bora kusamehewa huyo mkosa basi asamehewe. Ikionekana bora kulipwa kisasi — ili asiye akazidi kuendelea na madhara hayo anayowafanyia wenziwe — basi alipizwe. Mara nyingine Dawa ya Moto ni Moto. Cha kwa Cha. Lakini isiwe jawabu ya "Cha" ni "Cha Nina" wala "Cha Nguruwe." Jawabu ya Cha ni Cha tu au kusamehe. Kuzidisha katika malipo hapana ruhusa.

44. Maelezo yake ni kama ya Aya ya 8 ya Sura hii.

48. Na wakipuuza (atawalipa Mwenyezi Mungu). Nasi hatukukupeleka uwe mwenye kuwalinda; (wewe kazi yako kuwafundisha tu), si juu yako ila kufikisha tu. Na kwa yakini tunapomuonjesha mwanadamu rehema kutoka kwetu huifurahia (bila ya shukrani); na kama ikiwafika dhara kwa sababu ya hayo iliyoyatanguliza mikono yao, mara mwanaadamu huyu anamkufuru (Mwenyezi Mungu kuwa hampi kheri).

49. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; Anaumba Apendavyo, Anampa Amtakaye watoto wa kike na Anampa Amtakaye watoto wa kiume.

50. Au huwachanganya (watoto) wa kiume na wa kike (kwa mtu mmoja), na Humfanya tasa Amtakaye; hakika Yeye ni Mjuzi, Muweza.

51. Na haikuwa kwa mtu kwamba Mwenyezi Mungu anasema naye ila kwa ilhamu (anayotiwa moyoni mwake) au kwa nyuma ya pazia (la kumsikilizisha sauti inayotokana na Mwenyezi Mungu pasina kumuona Mwenyezi Mungu) au humtuma Mjumbe, (Jibrili); naye humfunulia (humletea Wahyi) kiasi anachotaka kwa idhini Yake; bila shaka Yeye ndiye aliye juu, Mwenye hikima.

52. Na namna hivi Tumekufunulia Wahyi kwa amri yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini wala imani; lakini tumefanya kitabu hiki (Qurani) ni nuru, ambayo kwa (nuru) hiyo Tunamuongoza Tumtakaye katika waja wetu. Na kwa yakini wewe unaongoza katika njia iliyonyoka:

53. Njia ya Mwenyezi Mungu ambaye ni vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi. Jueni kuwa mambo yote yanarudi kwa Mwenyezi Mungu.

فَإِنْ أَعْرَضُوا فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا
إِنْ عَلَيْكَ إِلَّا الْبَلَدُ وَإِنَّا إِذَا أَذَقْنَا الْإِنْسَانَ
مِمَّا رَحِمْنَا قَرَرًا يَفْرَحُ بِهَا وَإِنْ تَصْبِهِمْ سَبِيلًا
قَدَمَتْ أَيْدِيهِمْ فَإِنَّ الْإِنْسَانَ كَفُورٌ ۝

لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَ الْأَرْضِ يُخْلِقُ مَا يَشَاءُ
يَهْبِئُ لِمَنْ يَشَاءُ إِنَّا لَهُ وَهَّابٌ لِّسَنَ الْكَوْكُورِ ۝

أَوْ يَرْجُهُمْ ذُكْرًا وَ إِنَاثًا وَيَجْعَلُ مَنْ يَشَاءُ
عَقِيْبًا إِنَّهُ عَلِيمٌ قَدِيرٌ ۝

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ يَكْلِمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ
وَرَاءَ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ رَسُولًا فَيُوحِيَ بِإِذْنِهِ
مَا يَشَاءُ إِنَّهُ عَلَى حَكِيمٍ ۝

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا
مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَكِن
جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَنْ نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا
وَلَئِكَ نَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ۝

صِرَاطُ اللَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
الْأَرْضِ أَلَا إِلَى اللَّهِ تَصِيرُ الْأُمُورُ ۝

49. Aya hizo zinaweka wazi kabisa hapa kuwa anayefanya Utasa na Kuzaa kwa wake na waume au wake watupu na waume watupu, ni Mwenyewe Mwenyezi Mungu, si kaburi la Sharif gani wala Sheikhe gani; wala si Pepo wa nani wala Pepo wa nani. Wala si kwa ajili ya Marogo ya nani wala Marogozu ya nani.


Mambo yote ni ya Mungu

Atakalo ndilo huwa

Ndiye Pweke Mwenye quwa

Mwenye amri na shani.

51. Makadiyani Wamepachikapachika chungu ya maneno katika hii Aya waliyoifanya ya 52 ili wampachikie Utume huyo mtu wao. Na tumeyajibu kwa urefu haya katika marejezo ya Aya ya 40 ya Suratul Ahzab.



Ina Aya 89

SURATUZ ZUKHRUF

Ina Makara 7

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Haa Mym.

حَمْدٌ

2. Naapa kwa Kitabu (hiki) kinachobainisha (kila linalohitajiwa).

وَالْكِتَابِ الْمُبِينِ

3. Bila shaka tumekifanya (kitabu hiki) kiwe kisomo (kilichoteremka) kwa (lugha ya) Kiarabu ili mfahamu.

إِنَّا جَعَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

4. Na kwa yakini hii (Qurani) katika (Lawhil Mahfudhi) — asili ya vitabu vyote vilivyotoka kwetu — ni kitabu kilichotukuka chenye (maneno ya) hikima.

وَاللَّهُ فِي أُمِّ الْكِتَابِ لَدَيْنَا لَعَلَّكُمْ تَكْتُمُونَ

5. Je! Tuwache kukukumbusheni kwa sababu mumekuwa watu mliopita kiasi (katika ubaya)?

أَفَنَضْرِبُ عَنْكُمْ الذِّكْرَ صَفْحًا أَنْ كُنْتُمْ قَوْمًا

مُتْسِفِينَ

6. Na tuliwapeleka Manabii wengi katika watu wa zamani.

وَكَمْ أَرْسَلْنَا مِنْ نَبِيٍّ فِي الْأَوَّلِينَ

7. Na hakuwajia Nabii yoyote ila walikuwa wakimfanyia stihzai (kuwadharau).

وَمَا يَأْتِيهِمْ مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ

8. Basi tuliwaangamiza (hao; ambao) waliokuwa na nguvu zaidi kuliko hawa (Makureshi). Na mifano ya (adhabu zilizowafika) watu wa zamani imekwisha fika (kwao Makureshi, lakini bado tu wanapinga).

فَاهْلَكْنَا أَشَدَّ مِنْهُمْ بَطْشًا وَمَضَى مَثَلُ الْأَوَّلِينَ

9. Na ukiwauliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Kwa yakini watasema: "Ameziumba (Mwenyezi Mungu) — Mwenye nguvu, Mjuzi"

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ

خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ

10. Ambaye amekufanyieni ardhi kuwa kama tandiko, na akakufanyieni njia ndani yake ili muongoze (mnakotaka).

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ مَهْدًا وَجَعَلَ لَكُمْ فِيهَا

سُبُلًا لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

11. Na ambaye ameteremsha maji mawinguni kwa kiasi, na kwayo tukaufufua mji uliokufa. Na namna hivi ndivyo mtakavyotolewa (Makaburini).

وَالَّذِي نَزَّلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ فَأَنْشَرْنَا بِهِ

بَلَدَةً مَيِّتًا كَذَلِكَ تُخْرَجُونَ

7. Analiwazwa Mtume kuwa yanayompata ndiyo yaliyowapata wenziwe, si kiroja tu hicho kufanyiwa yeye.

12. Na ambaye amecumba dume na jike katika kila kitu na akakufanyieni marikebu na wanyama mnaowapanda

13. Ili mkae uzuri migongoni mwao, kisha mkumbuke neema za Mola wenu mnapokaa sawasawa juu yao na museme: "Ametukuka Mwenyezi Mungu aliyetutiishia haya na tusingaliweza kutenda haya wenyewe"

14. "Na bila shaka sisi tutarudia kwa Mola wetu."

15. Na wanamfanyia katika waja Wake sehemu (wakasema kuwa viumbe hivyo ni watoto wa Mungu). Kwa hakika mwanaadamu ni mkanushaji fadhila aliye dhahiri.

16. Oh! Amejichukulia watoto wanawake katika vile alivyoviumba, na kukuchagulieni nyinyi watoto wanaume?

17. Na anapobashiriwa mmoja wao kwa yale aliyompigia mfano Mwingi wa rehema, (yaani akiambiwa amezaa mtoto mwanamke), uso wake huwa mweusi na huhuzunika sana.

18. Oh! Aliyelelewa katika mapambo, naye katika mabishano hawezi kusema kwa bayana (ndio mnampa Mwenyezi Mungu)!, (yaani watoto wanawake).

19. Na wanawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa rehema (watukufu), kuwa wanawake. Je! Wameshuhudia kumowa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wataulizwa!

20. Na husema: "Angalipenda Mwingi wa rehema tusingewaabudu hao (masanamu. Ametuandikia Mwenyewe haya Mwenyezi Mungu, basi anayapenda)." Hawana ilimu kwa haya (wanayoyasema); hawasemi ila maneno ya kuvurumiza tu.

21. Je, tumewapa Kitabu kabla ya hiki, wakawa wameshikamana nacho? (Wanapata hayo wanayoyasema katika kitabu hicho?)

22. Bali wanasema: "Hakika sisi tuliwakuta baba zetu (wazee wetu) juu za dasturi (zao makhsusi), na sisi tunafuata nyayo zao."

وَالَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلْكِ وَالْأَنْعَامِ مَا تَرْكَبُونَ ﴿١٢﴾

لِتَسْتَوُوا عَلَى ظُهُورِهِ ثُمَّ تَذْكُرُوا نِعْمَةَ رَبِّكُمْ إِذَا اسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ وَتَقُولُوا سُبْحَانَ الَّذِي سَخَّرْنَا هَذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ ﴿١٣﴾

وَأَنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴿١٤﴾

وَجَعَلُوا لَهُ مِنْ عِبَادِهِ جُزْءًا إِنَّا لِلْإِنسَانِ أَفْكٌ ﴿١٥﴾

أَمْ آتَاخَذُ مِنْهَا يَخْلُقُ بَنَاتٍ وَأَصْفَكُمْ بِالْبَنِينَ ﴿١٦﴾

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ بِمَا صَرَبَ لِلرَّحْمَنِ مَثَلًا ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿١٧﴾

أَوْ مَن يَنْشَأُ فِي الْحَبْلَةِ وَهُوَ فِي الْخِصَامِ غَيْرُ مُبِينٍ ﴿١٨﴾

وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبْدُ الرَّحْمَنِ إِنَاءً أَشْهَدُوا خَلْقَهُمْ سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ وَيُسْأَلُونَ ﴿١٩﴾

وَقَالُوا لَوْ شَاءَ الرَّحْمَنُ مَا عَبَدْنَاهُمْ مَا لَهُمْ بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ إِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٢٠﴾

أَمْ آتَيْنَاهُمْ كِتَابًا مِّن قَبْلِهِ فَمُتُّ بِهِ مُتَمِّكُونَ ﴿٢١﴾

بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّهْتَدُونَ ﴿٢٢﴾

13. Hava ni maneno yaliyonuiwa kuyasema ukishakaa vizuri juu ya kipando chochote.

16. Waarabu walikuwa wakichukia kuzaa watoto wanawake, na wao wakisema kuwa Mwenyezi Mungu ana watoto wanawake.

22. Huu ndio ukorofi wa kila wanaoambiwa la haki wasikubali kufuata. Hoja yao: "Tumeyakuta haya kwa

23. Na kadhalika hatukupeleka Muonyaji katika mji wowote ila matajiri wake walisema: “Kwa yakini tuliwakuta baba zetu juu ya dasturi (zao makhsusi), na hakika sisi tutafuata nyayo zao.”

24. Akasema (huyo Mtume wao): “Hata kama nakuleteeni (dasturi) yenye uwongofu bora kuliko mliyowakuta nayo baba zenu (mtaendelea na dasturi ya wazee wenu)?” Wakasema: “Sisi tunayakataa tu hayo mliyotumwa (mlivokuia) navo.”

25. Basi Tukawapatiliza Angalia ulikuwaje mwi-sho wa wale waliokadhibisha!

26. Na (wakumbushe) Ibrahimu alipomwambia baba yake na watu wake: “Bila shaka mimi ninajitenga mbali na hayo manyoyaabudu

27. Isipokuwa yule aliyeniumba; kwa yakini Yeye ataniongoa.”

28. Na akalifanya (neno) hili ni neno lenye kubaki katika kizazi chake ili warejee (katika tamko hili).

29. Bali niliwastarehesha hawa na baba zao (wazee wao) mpaka ukawajia ukweli na Mtume anayebainisha (ya haki).

30. Na ulipowajia ukweli (wetu) walinena: “Huu ni uchawi, na hakika sisi tunaukanusha.”

31. Na walisema: “Kwa nini hii Qurani haikuteremshwa juu ya mtu mkubwa katika miji miwili (yetu hii ya Makka na Taif? Kwa nini akapewa maskini huyu)?”

وَكَذَلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِنْ نَذِيرٍ
إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهُمْ إِنَّا نَجِدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ
وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُقْتَدُونَ ﴿٢٣﴾

قُلْ أَوَلَوْ جِئْتُكُمْ بِآهْدَىٰ مِمَّا وَجَدْتُمْ عَلَيْهِ
آبَاءَكُمْ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ ﴿٢٤﴾

فَاتَّبَعْنَاهُمْ فَأَنْظِرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٥﴾

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي
بَرَاءٌ مِمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٢٦﴾

إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ ﴿٢٧﴾

وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ لَعَلَّهُمْ
يَرْجِعُونَ ﴿٢٨﴾

بَلْ مَنَعْتَ هَؤُلَاءِ وَ آبَاءَهُمْ حَتَّىٰ تَخْرُجَهُمُ
الْأَرْضَ وَرَسُولٌ مُبِينٌ ﴿٢٩﴾

وَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ وَإِنَّا بِهِ
كَافِرُونَ ﴿٣٠﴾

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنَ
الْقُرَيْشِيِّينَ عَظِيمٍ ﴿٣١﴾

waliotutangulia. Haya ndiyo asli. Yenu hayo Mambo leo. Msepere, ghafi hayo, si safi.” Na jawabu pia ndizo kama hizo wanazopewa. Nao hawakubali kusikia. Basi wenyewe watajionea.

31. Basi haya ndiyo waliyo nayo wanaadamu — hata sisi tunaajita Waislamu. Mizani yetu ya kumpimia mtu ni Nasabu na Mali. Aliye na haya basi ndiye anayestahiki kila kitu. Ndiyo hapa Maqureshi wanasema kwamba Lau kuwa huo Utume anaosema Nabii Muhammad ni wa kweli, basi asingepewa (a) yatima yeye; (b) fakiri. Angepewa ima Walyd bin Mughyra Al Makhzumi, (ami yake Abu Jahl) katika nchi ya Makka, au akapewa — katika nchi ya Taif — Urwa bin Masuud Ath Thaqafy, anayekhusika na Bani Umayya pia. Basi wanaambiwa hapa kuwa Uislamu hautazami Nasaba wala Mali. Uislamu unatazama nyoyo na amali. Basi natuache kujiona kwa Nasaba au

kwa Mali, ukasema:

Kitu kimevunja nguu
Kitu hukukweza juu
Kitu jani la tambuu
Mwenye kitu hana ila
Ukisema hivyo utajibiwa hivi:
Kitu usikite kitu
Kina vihendo kwa watu
Jino la ndovu ni kitu
Majibu tambua wewe

Na milima ikalala
Usifikwe na madhila
Atowaye ni jamala
Inshaallahu Taala.

Ingawa unacho wewe
Na kutaka wakuondowe
Huchongea auwawe
Utahadhari na kitu.

32. (Basi Mwenyezi Mungu anasema:) “Je, wao wanaigawa rehema ya Mola wako (wakampa wampendaye na wakamnyima wamtakaye?)” Sisi tumewagawanyia maisha yao katika uhai wa dunia na tumewainua baadhi yao daraja kubwa juu ya wengine; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wengine kuwa watumishi wao. Na rehema za Mola wako ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya.

33. Na kama isingekuwa watu watakuwa kundi moja wote, bila shaka Tungalifanya dari za nyumba za watu wanaomkufuru Mwingi wa rehema kuwa za fedha, na ngazi wanazopandia (pia za fedha).

34. Na milango ya nyumba zao na vitanda (mako-chi yao) vya kugemea kwao, (pia vyote vingekuwa vya fedha)

35. Bali na dhahabu (pia); lakini hayo si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu, na Akhera iliyo kwa Mola wako ni ya wenye kumcha Mwenyezi Mungu.

36. Anayeyafanyia upofu maneno ya Mwingi wa rehema tunamwekea Shetani kuwa rafiki yake, (kuwa mwenziwe)

37. Na wao wanawazuilia na njia (za kheri) na (wenyewe) wanadhani ya kwamba wameongoka.

38. Hata atakapotujia (siku ya Kiama, akawa anatiwa Motoni) atasema (kumwambia shetani): “Laiti ungalikuwa (mbali) umbali wa mashariki na magharibi baina yangu na wewe.” Na rafiki mbaya ulioje wewe! (Leo unanitia Motoni!).

39. (Na Mwenyezi Mungu atawaambia): “Haitakufaeni leo — mlivyodhulumu (nafsi zenu) — kwamba nyinyi mnashirikiana katika adhabu. (Kufa kwa jamaa si arusi, Uwongo maneno hayo).”

40. Je! Unaweza kuwasikilizisha viziwi, au unaweza kuwaongoa vipofu na waliyomo katika upotofu (upotevu) ulio wazi?

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ
مَعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ فَوْقَ
بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِّيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا حُرِّيًّا
وَرَحْمَتُ رَبِّكَ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٣٢﴾

وَلَوْلَا أَن يَكُونَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً لَّجَعَلْنَا لِمَن
يَكْفُرُ بِالرَّحْمَنِ لِيُوقِعَهُمْ سَفَافًا مِّنْ فَضْلِهِ وَمَعَارِجَ
عَلَيْهَا يَطْهَرُونَ ﴿٣٣﴾

وَلِيُوقِعَهُمْ أَرْبَابًا وَسُرَرًا عَلَيْهَا يَتَكَبَّرُونَ ﴿٣٤﴾

وَرُحُفًا وَإِن كُنَّا لَمَتَاءَ الْحَيَاةِ
الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٣٥﴾

وَمَنْ يَعْشُ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقَيِّضْ لَهُ شَيْطَانًا
فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿٣٦﴾

وَأَنَّهُمْ لَبَصَدُوتٌ مِّنَ السَّبِيلِ وَيَجْسَبُونَ أَنَّهُمْ
مُهْتَدُونَ ﴿٣٧﴾

حَتَّى إِذَا جَاءَنَا قَالَ يَلَيْتَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ بَعْدَ
الْمَشْرِقَيْنِ فَيُشَرِّقُونَ الْقَرَيْنَ ﴿٣٨﴾

وَلَنْ يَنْفَعَكُمْ أَيْوَمَ إِذْ ظَلَمْتُمْ أَنْفُسَكُمْ فِي
الْعَذَابِ مُشْتَرِكُونَ ﴿٣٩﴾

أَفَأَنْتَ تُسْمِعُ الصُّمَّ أَوْ تَهْدِي الْعُمْى وَمَنْ كَانَ
فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٤٠﴾

Mume huwa ana kitu
Akenda kwa mso kitu
Wakataajabu watu
Majibu tambua wewe

Asifurahi mkewe
Ukatulia moyowe
Hakika wasiijuwe
Utahadhari na kitu.

Na haya waliyoyapinga Maqureshi kwa Nabii Muhammad katika Aya hii ndiyo aliyoyapinga Firauni kwa Nabii Musa katika Aya ya 51 na za baada yake.

41. Na kama tukikuondoa (ulimwenguni kabla hukuona adhabu yao, usiwe na shaka). Sisi tutajilipiza kisasi (chetu) kwao

42. Au tutakuonyesha tuliyowaahidi, (Utaona kwa macho yako mwenyewe kabla hujafa). Nasi bila shaka tuna uweza juu yao.

43. Basi yashike yaliyofunuliwa kwako; bila shaka wewe umo katika njia iliyonyoka.

44. Na kwa yakini haya ni ukumbusho kwako na kwa watu wako, na karibuni hivi mtaulizwa.

45. Na kawaulize Mitume wetu tuliwaleta kabla yako: "Je! tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Mwingi wa rehema?"

46. Na bila shaka tulimtuma (tulimpeleka) Musa na Aya zetu kwa Firauni na wakuu wa uma wake, na akasema: "Kwa yakini mimi ni Mjumbe wa Mola wa walimwengu."

47. Lakini alipowafikia na hoja zetu, mara walizicheka (wasiziamini!).

48. Na hatukuwaonyesha hoja yoyote ila hiyo ilikuwa kubwa zaidi kuliko ile mwenziwe (iliyotangulia; na juu ya hivi hawakuamini). Na tukawakamata kwa adhabu (zetu, moja baada ya moja) ili warudi (kwetu).

49. Na walisema (kwa stihzai kumwambia Nabii Musa): "Ewe mchawi! Tuombe kwa Mola wako kwa ile ahadi aliyokupa, (akitundoshea adhabu hii ya safari hii), kwa yakini tutakuwa wenye kuongoka."

50. Basi tukiwaondolea adhabu hiyo mara huvunja tena. (Na vivyo hivyo kila siku).

51. Na Firauni alitangaza kwa watu wake, akanena: "Enyi watu wangu! utawala wa Misri si wangu, na pia mito hii ipitayo mbele yangu (si yangu)? Je! Hamuoni?"

52. "Au mimi si bora kuliko huyu (Musa) aliye mnyonge wala hawezi kusema waziwazi?"

53. "Basi mbona hakuvisiwa vikuku vya dhahabu, au kuja Malaika pamoja naye wakimuandama (wakimfuata kila mahala kama kweli Mtume)?"

54. Na kawachezea watu wake, nao wakamtii, kwa hakika wao walikuwa watu wenye kutoka katika taa (ya Mwenyezi Mungu; maasi).

فَأَمَّا نَذَهَبَ بِكَ فَأَنَا مِنْهُمْ مُتَتَّبِعُونَ ﴿٤١﴾

أَوْ نُرِيَنَّكَ الَّذِي وَعَدْنَاهُمْ فَأَنَا عَلَيْهِمْ مُقْتَدِرُونَ ﴿٤٢﴾

فَأَسْتَمِعِ بِالَّذِي أُوحِيَ إِلَيْكَ إِنَّكَ عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٤٣﴾

وَأَنَّهُ لَذِكْرُكَ لَكَ وَلِقَوْمِكَ وَسَوْفَ تُنْصَلُونَ ﴿٤٤﴾

وَسَأَلَ مَنْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ إِلَهًا يُعْبَدُونَ ﴿٤٥﴾

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَى بِآيَاتِنَا إِلَى فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ فَقَالَ إِنِّي رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٦﴾

فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِآيَاتِنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَصْتَكِبُونَ ﴿٤٧﴾

وَمَا يُرِيدُكُمْ مِنْ آيَةٍ إِلَّا هِيَ أَكْبَرُ مِنْ أُخْتِهَا ۚ وَأَخَذْنَاهُمْ بِالْعَذَابِ لَأَعْلَهُمْ يُجْجَعُونَ ﴿٤٨﴾

وَقَالُوا يَا إِلَهَ السَّجَرِ ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ ۖ إِنَّا لَمُهْتَدُونَ ﴿٤٩﴾

فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمْ الْعَذَابَ إِذَا هُمْ يَنْتَكِبُونَ ﴿٥٠﴾

وَنَادَى فِرْعَوْنُ فِي قَوْمِهِ قَالَ يُقَوْمِ أَلَيْسَ لِي مُلْكٌ مِصْرَ وَهَذِهِ الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِنْ تَحْتِي ۚ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٥١﴾

أَمْ أَنَا خَيْرٌ مِنْ هَذَا الَّذِي هُوَ مَهِينٌ وَلَا يَكَادُ يُبِينُ ﴿٥٢﴾

فَلَوْلَا أُلْقِيَ عَلَيْهِ أَسْوِرَةٌ مِنْ ذَهَبٍ أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَائِكَةُ مُقْتَرِنِينَ ﴿٥٣﴾

فَأَسْتَخَفَّ قَوْمَهُ ۖ فَاطَاعُوهُ ۖ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٥٤﴾

55. Basi walipotukasirisha tuliwapatiliza tukawagharikisha wote.

فَلَمَّا اسْتَفْزَنَّا انْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

56. Kisha tukawafanya kuwa mfano, (kumbukumbu) na hadithi kwa watu wanaokuja baada yao.

﴿٥٦﴾ فَجَعَلْنَاهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِّلْآخَرِينَ ﴿٥٦﴾

57. Na alipopigiwa mfano mwana wa Mariamu, (Nabii Isa), mara watu wako wakaupigia kelele.

وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٥٧﴾

58. Wakasema: "Je! miungu yetu ni bora au yeye?" Hawakuelezi hayo ila kwa kujadiliana tu; bali hao ni watu wagomvi (tu; hawataki ila ushindani tu).

وَقَالُوا آلَهِنَا خَيْرٌ أَمْ هُوَ مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ ﴿٥٨﴾

59. Hakuwa (Nabii Isa) ila ni mja tuliymneemesha na tukamfanya mithali (nzuri) kwa wana wa Israili.

إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّلْبَنَىٰ ۖ أَسْرَآءِيلَ ﴿٥٩﴾

60. Na kama tungalipenda tungewafanya Malaika (kuwa wakazi) wa ardhi hii badala yenu.

وَلَوْ شَاءَ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ ﴿٦٠﴾

61. Na kwa kweli (Yeye Nabii Isa) ni alama ya Kiama (kuwa kinaanza kutukaribia); msikifanyie shaka na nifuatani. Hii ndiyo njia iliyonyoka.

وَأِنَّهُ لَعِلْمٌ لِّلْآخِرَةِ فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا وَاتَّبِعُونِ ۚ هَٰذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

62. Wala asikuzuieni shetani; bila shaka kwenu yeye ni adui aliye dhahiri.

وَلَا يَصْدَقُكُمْ الشَّيْطَانُ ۚ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦٢﴾

63. Na alipofika Isa kwa dalili zilizo wazi, alisema: "Nimekujieni na ilimu (yenye nafuu na nyiye), na ili nikuelezeni baadhi ya yale mliyohitalifiana; basi Mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini."

وَلَمَّا جَاءَ عِيسَىٰ بِالْبَيِّنَاتِ قَالَ قَدْ جِئْتُكُمْ بِالْحِكْمَةِ وَلِأُبَيِّنَ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي تَخْتَلَفُونَ فِيهِ ۚ فَأَتَقُوا اللَّهَ وَاطِيعُوا ۖ ﴿٦٣﴾

58. Walipoambiwa makafiri wa Kiarabu kuwa watatiwa motoni pamoja na hayo masanamu yao wanayoyaabudu walisema: "Basi na Nabii Isa atatiwa Motoni pamoja na hao masanamu wanayoyaabudu." Hapa wanajitia pambani kusudi — imekhusu nini kutiwa Motoni Nabii Isa, na hali ya kuwa mtu mwema wala hakuwatuma wamuabudu. Ama masanamu yao hayo yakitiwa Motoni hapana kitu; ni mawe tu; wala hayahisi kitu.

61. Wameigeuza dhamiri (pronoun) ya *Wainnahu* yaani "Na yeye Nabii Isa." Wao wanasema "Na hii Qurani; ili kukataa yale maneno aliyoyasema Mtume ya kuwa Nabii Isa atakuja mwisho wa ulimwengu. Na tumeitaja kauli hii na hoja zake mara nyingi. Wao walipoirejeza ile Dhamiri katika Qurani wamesema kuwa: "Ndiyo kauli iliyoshikwa na Imam Hasan na watu wengine (Tafsir Maalimut Tanzyl)." Wameandika hivi kuonyesha mawili. Kuwa (a) mwenye Ma'alimut Tanzyl amekubali na (b) Kuwa imesemwa na Imam Al Hasan na wengi wengineo. Na hali ya kuwa waongo katika yote mawili. Kauli hiyo wameisema watu watatu tu: Yeye Hasan al Bisry na Qatada na Ibn Jubeyr, kama ilivyo katika sahifa 88 ya Juzuu ya 25 ya Ruuhul Maany, wanayojidai kuwa wanaifuata. Na akasema huyu Mwenye Ruuhul Maany kuwa kufanya hivi ni makosa; na akataja sababu ya kuwa ni makosa. Na wafasiri wengine wamefanya vihi hivi. Wao wanajidai kuwa mwenye Ma'alimut Tanzyl kaikubali!

Na wakaandika: "Kama tukubali ya kuwa neno 'ilimu' ni alama, basi katika Aya ya 86 ya Sura hii Mwenyezi Mungu anasema alama ya Kiama iko kwake. . ." Tunawambia: "Ndiyo alama za kuja Kiama ziko kwake; na moja ya alama hizo ni kuja Nabii Isa." Na wakaongezea uwongo wao: "na si kama itakuja, bali watu ndio watarudishwa katika alama hiyo." Haya "si kama itakuja" hayamo katika hiyo Aya wanayoisema kuwa ya 86. Wameyaongezea wao tu haya ili kuzidi kupoteza. Watazidi kupotea wenyewe tu, si watawapoteza Waislamu wanaojua dini yao.

64. "Kwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mola wangu na Mola wenu; basi Muabuduni; hii ndiyo njia iliyonyoka."

65. Lakini makundi kwa makundi yao yalihitalifiana wao kwa wao, basi kutawathubutikia wale waliodhulumu (nafsi zao) kuangamia kwa adhabu ya siku iumizayo.

66. Wanangoja nini ila Kiama tu kuwajia kwa ghafula, hali hawatambui.

67. Marafiki siku hiyo watakuwa maadui wao kwa wao (kwani walikuwa wakisaidiana katika maasi; na sasa wanajuta), ila wale (marafiki) waliokuwa wacha Mungu.

68. Enyi waja wangu (mlio wazuri)! Hamtakuwa na hofu siku hiyo wala hamtahuzunika.

69. (Waja wangu) Ambao waliziamini Aya zetu na walikuwa Waislamu kamili.

70. Ingieni Bustanini (Peponi) nyinyi na wake zenu; mtafurahishwa (humu).

71. Watakuwa wanapitishiwa sahani za dhahabu na vikombe (vya dhahabu); na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele.

72. Na hii ni Bustani, (Pepo) mliyorthishwa kwa hayo mliyokuwa mkiyafanya.

73. Muna (nyinyi) humo matunda mengi mtakayoyala.

74. Kwa hakika maasi watakaa katika adhabu ya Jahanamu.

75. Hawatapumzishwa nayo (adhabu hiyo); na humo watakata tamaa.

76. Wala sisi hatukuwadhulumu, bali wao wenyewe walikuwa madhalimu (wa nafsi zao).

إِنَّ اللَّهَ هُوَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَأَعْبُدُوا هَذَا صِرَاطَ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٣﴾

فَاخْتَلَفَ الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ ۖ قَوِيلٌ لِّلَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ عَذَابِ يَوْمِهِمُ الْأَلِيمِ ﴿١٤﴾

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٥﴾

الْأَخِلَّاءُ يَوْمَئِذٍ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ إِلَّا الْمُتَّقِينَ ﴿١٦﴾

يُعْبَادُ لَا خَوْفَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ وَلَا أَنتُمْ تَخَزُنُونَ ﴿١٧﴾

الَّذِينَ آمَنُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿١٨﴾

أَدْخِلُوا الْجَنَّةَ أَنْتُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ تُحْبَرُونَ ﴿١٩﴾

يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِصَفَافٍ مِّنْ ذَهَبٍ وَأَكْوَابٍ ۖ وَفِيهَا مَا تَشْتَهِيهِ الْأَنفُسُ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ ۖ وَأَنْتُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٠﴾

وَتِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢١﴾

لَكُمْ فِيهَا فَاكِهَةٌ كَثِيرَةٌ مِّنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٢٢﴾

إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّهِينٍ خَالِدُونَ ﴿٢٣﴾

لَا يُفْتَرُ عَنْهُمْ وَهُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٢٤﴾

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا هُمُ الظَّالِمِينَ ﴿٢٥﴾

67. Hakuharibika mwanamume yoyote yule ila kwa kuchochewa na rafiki yake mbaya. Wala hakuharibika mwanamke yoyote yule ila kwa shoga (rafiki) yake mbaya. Basi natutahadhari na marafiki na mashoga (marafiki) wabaya. Mapenzi ya hapa tu duniani, kisha yatakuwa machukiano makubwa kabisa baina yao siku ya Kiama, kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 25 ya *Suratul Ankabut* Bali wataanza kuchukiana tangu hapa kwa mabaya yatakayowafika hapa kabla ya Akhera.

Fulani nalikwambiya
Ya watu walo wabaya
Umekwisha kuingiya

Wacha suhuba
Huo ukuba
Kwenye misiba.

77. Nao watapiga kelele (kumwambia yule Malaika anayewaadhibu waseme): “Ee Malik! Naatufishe Mola wako!” (Malik) aseme: “Bila shaka mtakaa humu humu.”

78. “Kwa yakini tulikuleteeni (maneno ya) haki, lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia haki.”

79. Ndiyo wameweza (wabaya hao) kupitisha amri (yao) au sisi ndio wapitishaji (wa kila tunalolitaka)? (Bali sisi ndio wapitishao tunayoyataka).

80. Au wanadhani ya kwamba hatusikii siri zao na minong’ono yao? Wapi! (Tunasikia sisi wenyewe); na Wajumbe wetu, (Malaika) wako karibu nao; wanayaandika.

81. Sema: “(Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema angalikuwa na mtoto ningekuwa wa kwanza wa kumuabudu (mtoto huyo kwa kuwa ni mtoto wa Mungu wangu).”

82. Ameepukana Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi — na hayo wanayomsifia.

83. Basi wawache wapige porojo na wacheze mpaka wakutane na siku yao wanayoahidiwa.

84. Na Yeye ndiye anayeabudiwa mbinguni na anayeabudiwa ardhini; naye ni Mwenye hikima, Mwenye ilimu.

85. Na ametukuka kweli kweli yule ambaye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ni wake, na uko kwake ujuzi wa (kuja) Kiama; na (nyote) mtarudishwa (mtarejeshwa) kwake.

86. Wala hawana uweza wa uombezi wale wanaowaomba (wanaowaabudu) badala Yake (Mwenyezi Mungu. Hakuna Mwenye kupewa uweza huo) ila wale wanaoikiri hii haki, wakaijua.

87. Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba? Kwa yakini yatesema: “Ni Mwenyezi Mungu.” Basi ni wapi wanakogeuziwa?

88. Na usemi wake (Nabii Muhammad wa kila mara) ni: “Ee Mola wangu! Kwa yakini hawa ni watu wasioamini. (Sijui niwafanyeje).”

89. Basi wasamehe wewe na uwambie (maneno ya) salama. (Labda mwisho wake watatambua). Hivi karibuni watajua.

وَنَادَا يَمْلِكُ لِيَقْضَ عَلَيْكَ رَبُّكَ قَالَ إِنَّكُمْ لَمُكْرُونَ ﴿٥٧﴾

لَقَدْ جِئْتُمْ بِالْحَقِّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَكُمْ لِلْحَقِّ كُرْهُونَ ﴿٥٨﴾

أَمْ أَرْبُومَا أَمْثَلَا مَبْرُومُونَ ﴿٥٩﴾

أَمْ يَحْسِبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ بَلَىٰ وَرُسُلْنَا لَدَيْهِمْ يَكْتُبُونَ ﴿٦٠﴾

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَابِدِينَ ﴿٦١﴾

سُبْحَنَ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٦٢﴾

فَذَرُهُمْ يَفْضَحُوا وَيَلْعَبُوا حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٦٣﴾

وَهُوَ الَّذِي فِي السَّمَاءِ إِلَهٌُ وَفِي الْأَرْضِ إِلَهٌُ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ ﴿٦٤﴾

وَتَبَارَكَ الَّذِي لَهُ مَلَكُوتُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۚ وَعِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ ۚ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٦٥﴾

وَلَا يَمْلِكُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ الشَّفَاعَةَ إِلَّا مَنْ شَهِدَ بِالْحَقِّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٦٦﴾

وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ فَأَلَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٦٧﴾

وَقِيلَ لَهُ يَرْبُ إِنَّ هَؤُلَاءِ قَوْمٌ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٨﴾

فَاصْفَعْ عَنْهُمْ وَقُلْ سَلَامٌ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٦٩﴾

89. Wanahimizwa Waislamu (a) wawasamehe waovu — kama yalivyokaririwa haya ndani ya Qurani nzima; na (b) kusema maneno ya salama hata wakiambiwa yasiyokuwa mazuri.



Ina Aya 59

SURATUD DUKHAN

Ina Makara 3

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Haa Mym.

حَمْدٌ

2. Naapa kwa Kitabu (hiki) kinachobainisha (kila linalohitajiwa).

وَالْكِتَابِ الْمُبِينِ

3. Kwa yakini tumeteremsha (Qurani) katika usiku uliobarikiwa — bila shaka Sisi ni waonyaji.

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ مُبَرَكَةٍ إِنَّا كُنَّا مُنْذِرِينَ

4. Katika (usiku) huu hubainishwa kila jambo la hikima

فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ

5. Ndiyo hukumu inayotoka kwetu; kwa hakika sisi ni waletao (Mitume ili wawaongoe viumbe).

أَمْرًا مِّنْ عِندِنَا إِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ

6. Ni rehema itokayo kwa Mola wako. Bila shaka Yeye ndiye Mwenye kusikia (na) Mwenye kujua

رَحْمَةً مِّنْ رَبِّكَ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

7. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake; ikiwa mnayo yakini (basi yakinisheni haya).

رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا إِنْ كُنْتُمْ مُّوقِنِينَ

8. Hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yeye, anahuisha na kufisha, Mola wenu na ni Mola wa wazee wenu (wote) wa mwanzo (na Mola wa kila kitu).

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ

أَبَائِكُمُ الْأَوَّلِينَ

9. Lakini hao (makafiri) wamo katika shaka na wanacheza tu.

بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ يَّالْعَبُونَ

10. Basi ingoje siku ambapo mbingu zitakapoleta moshi ulio dhahiri

فَارْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُخَانٍ مُّبِينٍ

11. Utakaowafunika watu; (wawe wanasema): "Hii ni adhabu iumizayo "

يُعْثِقُ النَّاسَ هَذَا عَذَابٌ أَلِيمٌ

3. Hii Laylatin Mubaarakatin. . . Fyhaa yafraqu kullu amriin Hakym. Dhahir shahir hapa kuwa siku hii imo katika mwezi wa Ramadhani kama yalivyobainishwa haya na Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika Aya ya 185 ya *Suratul Baqarah*. Basi si kweli hayo maneno yanayosemwa kuwa huo ni usiku wa kuamkia mwezi 15 Shaaban wanaouita *Qasmatul Rizq*. Na hiyo dua inayosomwa usiku huo inapingwa na wanavyuoni wajuzi wa kweli kwani muna maneno yanayopingana na Qurani. Wala hayakuwa haya — ya mikutano hiyo ya usiku huo — katika zama za mwenyewe Mtume wala Masahaba wala Taabiina. Basi tujiepushe na Mabidaa.

10-16. Yanatajwa baadhi ya yaliyowafika Maqureshi kwa kumkadhibisha Mtume. Njaa kubwa kabisa iliawafika hata wakaja kwa Mtume kuomba nusura. Na Mtume kwa huruma yake aliwaombea. Na inatajwa namna walivyopata mashambulio ya vita vya Badr.

12. "Mola wetu! Tuondolee adhabu (hii) hakika tutaamini"

13. Nini faida ya kukumbuka kwao (sasa)? Na alikwisha wajia Mtume abainishaye

14. Wakampa kisogo na wakasema: "Amefunzwa (na watu haya, hakuletewa Wahyi; na) ni mwendawazimu."

15. Kwa yakini Sisi tutaiondoa adhabu kidogo (lakini) nyinyi mtarudia (makosa yenu).

16. Na (wakumbushe) siku tutakayoshambulia mshambulio mkubwa: bila shaka Sisi ni wenye kutesa (kweli kweli).

17. Na hakika kabla yao Tuliwafanyia mtihami watu wa Firauni, na aliwajia Mtume ahishimiwaye

18. (Akasema); "Nipeni waja wa Mwenyezi Mungu, (hawa Mayahudi nitoke nao hapa Misri mnapowataabisha). Kwa hakika mimi ni Mtume muaminifu (niliyeletwa kwenu)"

19. "Na msitakabari mbele ya Mwenyezi Mungu; mimi kwa yakini nitakuleteeni dalili zilizo wazi (za kuonyesha Utume wangu)."

20. "Nami najikinga kwa Mola wangu na (ndiye) Mola wenu (pia) ili msinipige mawe."

21. "Na kama hamniamini, basi jitengeni nami, (msinidhuru)."

22. Ndipo akamuomba Mola wake kwamba "Hawa ni watu waovu, (nihami nao)."

23. (Mwenyezi Mungu akamwambia): "Basi nenda pamoja na waja wangu (hawa Bani Israil) usiku, na mtafuatwa kwa yakini"

24. "Na iache bahari (vivyo hivyo imeachana baada ya kwishakupita wewe na watu wako, usiifanye kukamatana tena mpaka apite Firauni na watu wake; wakipita itaambatana waghariki); hakika wao ni jeshi litakalozamishwa"

رَبَّنَا اكشِفْ عَنَّا الْعَذَابَ إِنَّا مُؤْمِنُونَ ﴿١٢﴾

أَنَّى لَهُمُ الذِّكْرَى وَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مُبِينٌ ﴿١٣﴾

لَقَدْ تَوَلَّوْا عَنْهُ وَقَالُوا مُعَلَّمٌ مَجْنُونٌ ﴿١٤﴾

إِنَّا كَاشِفُو الْعَذَابِ قَلِيلًا إِنَّكُمْ عَائِدُونَ ﴿١٥﴾

يَوْمَ نَبْطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرَى إِنَّا مُنتَقِمُونَ ﴿١٦﴾

وَلَقَدْ فَتَنَّا قَبْلَهُمْ قَوْمَ فِرْعَوْنَ وَجَاءَهُمْ رَسُولٌ كَرِيمٌ ﴿١٧﴾

أَن أَدُّوا إِلَيَّ عِبَادَ اللَّهِ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿١٨﴾

وَأَن لَّا تَعْلَوْا عَلَى اللَّهِ إِنِّي آتِيكُمْ بِسُلْطَانٍ مُبِينٍ ﴿١٩﴾

وَاللَّيْلُ عَدَّتْ بِرَبِّي وَأَرْسَلْنَاكَ أَن تَرْجِعُونَا ﴿٢٠﴾

وَلَوْ لَمْ تَأْمُرْنَا لَعَنَّا لَوْلَا ﴿٢١﴾

فَدَعَا رَبَّهُ أَنِ مَوْلَاةٌ قَوْمٍ مُّجْرِمُونَ ﴿٢٢﴾

فَأَسْرِ بِمَا بِدِي كَيْلًا إِنَّكُمْ تُسَبَّحُونَ ﴿٢٣﴾

وَأَتْرِكُ الْبَهِرَ رَهْوَماً إِنَّهُمْ جُنْدٌ مُّعْرَقُونَ ﴿٢٤﴾

24. Makadiyani hapa katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 25 wametia ukafiri wa kumkanusha Mwenyezi Mungu kwa miujiza anayoitaja. Mwenyezi Mungu amekithirisha kutaja muujiza huu wa Nabii Musa wa kuipiga bahari ikapasuka, akapita salama, yeye na watu wake. Wao — kwa kumsuta kwao Mwenyezi Mungu — wanasema kuwa maji yalikuwa yamekupwa! Hakuna mfasiri wa Qurani wala wa lugha ya Kiarabu tu aliyesema kuwa *Rahwan* = yamekupwa. Ukafiri mkubwa kabisa huu wa kusingizia uwongo kila kitu — tangu viumbe vyake Mwenyezi Mungu mpaka Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

25. Mabustani mangapi na chemchem ngapi waliziacha (baada ya kugharikishwa)

كَمْ تَرَكُوا مِنْ جَدَّتٍ وَعُيُونٍ ۝

26. Na mimea na mahali pazuri!

وَزُرُوعٍ وَ مَقَامٍ كَرِيمٍ ۝

27. Na neema (kubwa kubwa) walizokuwa wakijistareheshea

وَنَعْمَةٍ كَانُوا فِيهَا فُكِهَيْنَ ۝

28. Namna hivi (tumewafanya) Na tukawarithisha haya watu wengine.

كَذَلِكَ تَدَاوَرَّتْهَا قَوْمًا آخَرِينَ ۝

29. Mbingu na ardhi hazikuwalilia. (Walio katika ardhi hawakuwalilia wala walio mbinguni kwani walikuwa watu wabaya). Wala hawakupewa muda (wa kurejea tena ulimwenguni).

فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ وَمَا كَانُوا مُنْظَرِينَ ۝

30. Na bila shaka tuliwaokoa wana wa Israili katika adhabu ya kuwadhalilisha

وَلَقَدْ نَجَّيْنَا بَنِي إِسْرَءِيلَ مِنْ الْعَذَابِ الْمِهِينِ ۝

31. Ya Firauni. Hakika yeye alikuwa jeuri (na) katika wenye kupindukia mipaka.

مِنْ فِرْعَوْنَ إِنَّهُ كَانَ عَلِيًّا مِنَ السَّرِيفِينَ ۝

32. Na tukawachagua (Mayahudi) kwa ujuzi (wetu) kuliko walimwengu (wengine wote).

وَلَقَدْ اخْتَرْنَاهُمْ عَلَىٰ عِلْمٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ۝

33. Na tukawapa katika mambo (yetu) mambo ambayo ndani yake muna neema (kubwa kubwa) zilizo dhahiri.

وَ اتَيْنَهُمْ مِنَ الْآيَاتِ مَا فِيهِ بَلَاءٌ مُبِينٌ ۝

34. Hakika hawa (makafiri) wanasema:

إِنْ هَؤُلَاءِ لَيَقُولُونَ ۝

35. Hakukuwa (kufa) ila ni mauti yetu (yaya haya) ya kwanza (tunayoyajua), wala sisi hatutafufuliwa."

إِنْ هِيَ إِلَّا مَوْتُنَا الْأُولَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُنْشَرِينَ ۝

36. "Basi warudisheni wazee wetu (waliokufa); ikiwa mnasema kweli (kuwa kuna kufufuka)!"

فَأَنذِرُوا يَا بَنِي إِدْرِمَ إِنَّكُمْ صَادِقِينَ ۝

Tena wakajidai kutaja Sura na Aya ili kuthibitisha uwongo huu, wakaandika:

(a) 2:51, yaani Aya *Waidh Faraqnaa Bikumul Bahr*. Na hali ya kuwa maana yake: "Kumbukeni tulipokupasulieni bahari." Iko wapi "kukupwa"?

(b) 7:137, yaani *Faaghraqnaahum Filyamm* = Tukawagharikisha baharini. Iko wapi "maji yalikutwa"?

(c) 8:55, yaani *Faaghraqnaa Aala Fir-aun* = Tuliwagharikisha Kina Firauni. Iko wapi "maji yalikutwa"?

(d) 20:78, yaani *Fadhrib Lahum Taryqan Fil Bahr* = Wapigie njia katika bahari. Iko wapi maji yalikutwa?

Hapa imeajwa khasa kuwa "Wapigie njia katika bahari" yaani kwa fimbo yako kama ilivyo katika Aya ya 63 ya *Suratush Shuaraa*.

(e) 20:81 Hamna hapa habari ya bahari! Sijui kwa nini wakaitaja na Aya hii. Wameitia ili wajaze farumu tu.

(f) 28:41, yaani *Fanabadhnaahum Filyamm* = Tukawatupa baharini. Na iko wapi hapa pia kuwa "maji yalikutwa"?

Wajasiri kweli kweli! Wanampinga Mwenyezi Mungu vivi hivi dhahir shahir! Mwenyezi Mungu anasema ameipiga bahari kwa fimbo yake — kama ilivyo katika Aya ya *Suratush Shuaraa* — wao wanasema maji yalikutwa!

29. Wema wakiondoka ulimwenguni husikitikiwa na wema wa mbinguni na wema katika ardhi. Na hufurahi kwa kuondoka watu wabaya.

37. (Mwenyezi Mungu anasema:) "Je! Wao ni bora au watu wa Tubba, (wafalme wa Yaman) na wale waliokuwa kabla yao? Tuliwaangamiza (wote hao); kwa yakini wao walikuwa waovu."

38. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo.

39. Hatukuviumba ila kwa haki, lakini wengi wao hawajui.

40. Kwa kweli siku ya Hukumu ni wakati uliowekwa kwa wao wote

41. Siku ambayo jamaa hatamfaa jamaa (yake kwa) chochote, wala hawatanusuriwa

42. Ila wale Mwenyezi Mungu atakaowarehemu. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu (na) Mwingi wa rehema.

43. Bila shaka mti wa Zakkum

44. Ni chakula cha (kuliwa na) maasi,

45. (Kwa umoto wake ni) kama shaba iliyoyayushwa; huchemka matumboni

46. Kama mchemko wa maji ya moto kabisa.

47. (Kuambiwe:) "Mkamateni (huyō asi) na mumtupe katikati ya Jahanamu."

48. "Kisha mwagieni juu ya kichwa chake (maji ya moto kabisa aonje) adhabu ya maji ya moto (ya kweli kweli)."

49. (Aambiwe:) "Onja! Ulikuwa (ukijidai kuwa) wewe ni mwenye nguvu; mhishimiwa! (Onyesha leo nguvu zako)."

50. "Hakika hii ndiyo ile (adhabu) mliyokuwa mkibishana, (mkiutilia shaka)."

51. Bila shaka wale wamchao Mwenyezi Mungu watakuwa katika mahali pa amani

52. Katika mabustani na chemchem

53. Watavaa hariri laini na hariri nzito; wakikabiliana (wanazungumza)

54. Hivi (ndivyo itakavyokuwa) na tutawaoza mahurilaini (Wanawake wa Peponi huko).

55. Humo watataka (na wapate) kila aina ya matunda, na wakae kwa amani

أَمْ خَيْرٌ أَمْ قَوْمٌ تُبْعِ وَأَلَّيْنِ مِنْ قَبْلِهِمْ
أَهْلَكْتَهُمْ إِنْهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ ۝

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا
لْعِينِينَ ۝

مَا خَلَقْنَاهُمْ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَكِنْ أَكْثَرُهُمْ لَا
يَعْلَمُونَ ۝

إِنَّ يَوْمَ الْقِيَامِ مِيقَاتُهُمْ أَجْمَعِينَ ۝
يَوْمَ لَا يُغْنِي مَوْلًى عَنْ مَوْلًى شَيْئًا وَلَا هُمْ
يُنصَرُونَ ۝

إِلَّا مَنْ رَحِمَ اللَّهُ إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ۝

إِنَّ شَجَرَتَ الزُّكُّومِ ۝
طَعَامُ الْآثِيمِ ۝

كَالْهَلِيلِ يَغْلَى فِي الْبُطُونِ ۝
كَغَلَى الْعَمِيمِ ۝

حُدُودَهُ قَاعَتَا لَوْاءٍ سَوَاءِ الْجَحِيمِ ۝

ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِنْ عَذَابِ الْحَمِيمِ ۝

ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ۝

إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ۝

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي مَقَامِ أَمِينٍ ۝
فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ۝

يَلْبَسُونَ مِنْ سُندُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ مُتَقَابِلِينَ ۝

كَذَلِكَ نُورُ رُوحَانِهِمْ بِحُورٍ عِينٍ ۝
يَدْعُونَ فِيهَا بِكُلِّ فَاكِهَةٍ آمِنِينَ ۝

43. Zakkum ni chakula cha Kimotoni, kitajulikana huko na hao watakaokila.

56. Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza, na atawalinda na adhabu ya Jahanamu.

لَا يَذُوقُونَ فِيهَا الْمَوْتَ إِلَّا الْمَوْتَةَ

57. Kwa fadhila zitokazo kwa Mola wako; huko ndiko kufaulu kukubwa.

الْأُولَىٰ، وَوَفَّيْنَاهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ ۝

58. Basi tumeifanya nyepesi hii (Qurani) kwa ulimi wako, (lugha yako ya Kiarabu) ili wakumbuke.

فَضْلًا مِّن رَّبِّكَ، ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ۝

وَمَا يَسَّرْنَاهُ بِلِسَانِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ۝

59. Ngoja tu, na wao wanangoja (pia).

فَلَا تَقْبَلْ لَهُمْ مَّرْتَبُونَ ۝



Aya 37

SURATUL JATHIYAH

(Imeteremka Makka)

Ina Makara 4

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Haa Mym.

حَمْدٌ ①

2. Uteremsho wa Kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, (na) Mwenye hikima.

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ①

3. Bila shaka katika mbingu na ardhi ziko alama kubwa (za kuonyesha kuwa yuko Mwenyezi Mungu), kwa ajili ya wanaoamini.

إِنَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِلْمُؤْمِنِينَ ①

4. Na katika umbo lenu na katika viumbe alivyovitawanya zimo alama (vile vile) kwa watu wenye yakini

وَفِي خَلْقِكُمْ وَمَا يَبُذُّ مِنْ دَابَّةٍ آيَاتٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ①

5. Na (katika) kupishana, (kufuatana) usiku na mchana na (katika) riziki aliyoteremsha Mwenyezi Mungu kutoka mawinguni, (mvua) na akaifufua kwayo ardhi baada ya kufa kwake, na katika mabadiliko ya pepo, zimo alama pia kwa watu wenye akili.

وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ رِزْقٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَتَصْرِيفِ الرِّيْحِ آيَاتٌ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ①

6. Hizi Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa ukweli; basi hadithi gani watakayoiamini baada ya (kupuuza hadithi ya) Mwenyezi Mungu na Aya zake?

تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَنْزَلُوهَا عَلَيْكَ يَا نَبِيَّ، قَبْلَ هَذِهِ حَدِيثٍ بَعْدَ اللَّهِ وَآيَاتِهِ يُؤْمِنُونَ ①

7. Kuangamia kutamthubutikia kila atungaye (azuwaye) uwongo, mwenye chungu ya madhambi

وَيَلْ لَّكُلِّ أَقَامٍ آثِمٌ ①

8. Anayesikia Aya za Mwenyezi Mungu zikisomwa juu yake, kisha anashikilia (yale yale aliyokatazwa) na anajivuna kama kwamba hakuzisikia; basi mpe habari ya adhabu iumizayo, (inayomngoja).

يَسْمَعُ آيَاتِ اللَّهِ تُتْلَى عَلَيْهِ ثُمَّ يُصِرُّ مُسْتَكْبِرًا كَأَن لَّمْ يَسْمَعْهَا، فَبَشِيرَةٌ بَعْدَ آيِ الْيَوْمِ ①

9. Na anapokijua (anapokisikia) kitu kidogo katika Aya zetu hukifanyia mzaha. Watu hao ndio watakaokuwa na adhabu idhalilishayo.

وَإِذَا عَلِمَ مِنْ آيَاتِنَا شَيْئًا اتَّخَذَهَا هُزُوًا، أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُهِينٌ ①

6. Basi khatari kubwa kabisa kuyaacha maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa maneno ya mtu mwengine.

10. Na nyuma yao iko Jahanamu (inawangoja). Na waliyoyachuma hayatawafaa hata kidogo, wala walinzi (waola) waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu (hawatawafaa vile vile); na watapata adhabu kubwa.

11. Huu ni uwongofu; na wale waliozikataa Aya za Mola wao watakuwa na adhabu kubwa yenye kutokana na adhabu iumizayo.

12. Mwenyezi Mungu Ndiye aliyekutiishieni bahari ili humo zipite marikebu kwa amri yake, na ili mtafute fadhila yake na mpate kushukuru.

13. Na Amekutiishieni, (ametia chini ya taa yenu) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini — vyote vimetoka kwake; bila shaka katika haya zimo alama (kubwa za neema za Mwenyezi Mungu juu yenu) kwa watu wanaofikiri.

14. Waambie wale walioamini wawasamehe wale wasioziogopa siku za Mwenyezi Mungu (za kuwatia adabu wabaya), ili awalipe watu kwa yale waliyokuwa wakiyachuma.

15. Mwenye kutenda wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake (mwenyewe), na mwenye kufanya uovu ni juu yake (mwenyewe pia); kisha mtarudishwa kwa Mola wenu.

16. Na kwa yakini tuliwapa wana wa Israili Kitabu na hukumu na unabii, na tukawapa vitu vizuri vizuri na tukawafadhilisha kuliko walimwengu wote (wa zama zao).

17. Na tukawapa maelezo dhahiri ya amri (yenu ya dini). Basi hawakuhitalifiana ila baada ya kuwajia ilimu. (Walihitalifiana) kwa husuda iliyokuwa baina yao. Hakika Mola wako atahukumu baina yao siku ya Kiama katika yale waliyokuwa wakihitalifiana.

مِنْ وَرَائِهِمْ جَهَنَّمُ وَلَا يُغْنِي عَنْهُمْ مَا كَسَبُوا شَيْئًا وَلَا مَا اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ أَوْيَاءً. وَ لَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ.

هَذَا هُدًى. وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ لَهُمْ عَذَابٌ مِّن رَّجَرٍ أَلِيمٌ.

اللَّهُ الَّذِي سَخَّرَ لَكُمُ الْبَحْرَ لِتَجْرِيَ الْفُلُكُ فِيهِ بِأَمْرِهِ وَ لَتَتَّبِعُوا مِنْ فَضْلِهِ وَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ.

وَ سَخَّرَ لَكُم مَّا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ. إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ.

قُلْ لِلَّذِينَ آمَنُوا يَغْفِرُوا لِلَّذِينَ لَا يَرْجُونَ أَيَّامَ اللَّهِ لِيَجْزِيَ قَوْمًا بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ.

مَنْ عَمِلْ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ، وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا. ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ.

وَ أَقَدْ آتَيْنَا بَنِي إِسْرَءِيلَ الْكِتَابَ وَ الْحُكْمَ وَ النَّبُوَّةَ وَ رَزَقْنَاهُمْ مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَ فَضَّلْنَاهُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ.

وَ آتَيْنَاهُمْ بَيِّنَاتٍ مِّنَ الْأَمْرِ مَّا اخْتَلَفُوا إِلَّا مِّنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَعِيًّا. بَيْنَهُمْ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَمَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ.

13. Aya hii inathubutisha yale aliyoyasema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 53 ya Surat Haa Mym Sajdah ya kuwa yanayosemwa na Qurani ni kweli tu. Hapa Mwenyezi Mungu anatwambia kuwa ametudhalilishia hata vilivyoko mbinguni. Ndipo kwanza sasa tunaona watu wanazishambulia sehemu za mbingu zilizo karibu yetu, kama walivyoichungua ardhi kila upande.

Wanataka nini zaidi la kuonyesha ukweli wa yaliyomo katika Qurani kuliko haya yanayodhihiri ukweli wake kila usiku uchapo! KWENDA MWEZINI NA UKWELI WA QURANI.

Khabari hii ya kwenda Mwezini imeleta ubishi mkubwa kwa Waislamu. Kwa hivi tumeonelea kuwa ni vizuri kuyaweka wazi mas'ala haya katika upande wa Dini.

Waislamu wanaitakidi kuwa Quran ni maneno ya Mwenyezi Mungu aliyomletea Mtume wake wa Mwisho, Nabii Muhammed ili aongezee viumbe.

Na akasema humo Dhahir Shahir kuwa kila kilichosemwa humo ni kweli — kimekuwa au kitakuwa. Kama ilivyo katika Aya ya 115 ya Suratul — An-Am inayosema, "Yametimia maneno ya Mola wako kwa Ukweli na

18. Kisha tumekuweka juu ya Sharia ya amri yetu, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wale wasiojua (kitu).

19. Kwa yakini hao hawatakufaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hakika madhalimu ni marafiki wao kwa wao (hapa ulimwenguni; lakini Akhera watachukiana). Na Mwenyezi Mungu ni rafiki wa wale wamchao.

20. Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu (wote); nazo ni uwongofu na rehema kwa watu wanao yakinisha.

21. Je! Wanafikiri wale waliofanya maovu kuwa tutawafanya kama wale walioamini na kutenda mema—kwamba maisha yao na mauti yao yawe sawa? Ni hukumu mbaya wanayoihukumu (ya kuwa wote watakuwa sawa).

22. Na Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi kwa haki na ili kila nafsi ilipwe yale iliyoyachuma; nao hawatadhulumiwa.

23. Je! Umemuona yule aliyefanya yale anayoyataka yeye, kuwa ndiye mungu wake; na Mwenyezi Mungu akamwacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi; na akapiga muhuri juu ya masikio yake na moyo wake; na kumtia kitanga machoni pake; basi nani atamwongoza baada ya Mwenyezi Mungu? Basi je hamkumbuki?

24. Na walisema: “Haukuwa (uhai) ila ni uhai wetu huu wa dunia, (hakuna mwengine); tunakufa na tunaishi, wala hakuna kinachotuangamiza isipokuwa (huu huu) ulimwengu; (kwani ndiyo ada yake kufisha na kuhuisha).” Lakini wao hawana ilimu ya hayo (wanayoyasema) wanadhani tu.

25. Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi hawana hoja ila kusema: “Waleteni baba zetu, (wazee wetu waliokufa) ikiwa nyinyi ni wasemao kweli (kuwa watu watafufuliwa)!”

26. Sema: “Mwenyezi Mungu anakupeni uhai, kisha anakufisheni, kisha atakukusanyeni siku ya Kiama — (siku ambayo) haina shaka; lakini watu wengi hawajui.”

Uadilifu,” na katika Sura nyinginezo. Na akasema kama ilivyo katika Aya ya 42 Surat Fussilat — kuwa haimkiniki kupatikana jambo humo ambalo litakuwa silo. Ilisema hivi: “(Kitabu hiki) hakijiwi na cha kubatilisha (kilichoyasema), si katika vitabu vilivyotangulia wala vinavyokuja nyuma.”

Na akasema kuwa vitakuwa vitu hivyo vilivyotajwa humo visivyotokea bado. Vitakuwa vionekane na Ulimwengu

ثُمَّ جَعَلْنَاكَ عَلَىٰ شَرِيعَةٍ مِّنَ الْأَمْرِ فَاتَّبِعْهَا وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ⑤

إِنَّهُمْ كَنُ يُغْنُوا عَنْكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۚ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ ۚ وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُتَّقِينَ ⑥

هَذَا بَصَائِرُ لِلنَّاسِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ⑦

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ اجْتَرَحُوا السَّيِّئَاتِ أَن نَّجْعَلَهُمْ كَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ۚ سَوَاءٌ مَّحْيَاهُمْ وَمَمَاتُهُمْ ۚ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ⑧

وَخَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ وَلِتُجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ⑨
أَفَرَأَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوَاهُ وَأَضَلَّهُ اللَّهُ عَلَىٰ عِلْمِهِ وَخَتَمَ عَلَىٰ سَمْعِهِ وَقَلْبِهِ وَجَعَلَ عَلَىٰ بَصَرِهِ غِشَاوَةً ۖ فَمَنْ يَهْدِيهِ فَمَنْ يَبْعِدِ اللَّهُ ۖ أَفَلَا تُدْرِكُونَ ⑩

وَقَالُوا مَا هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَا إِلَّا الدَّهْرُ ۚ وَمَا لَهُمْ بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ ۚ إِنْ هُمْ إِلَّا يَظُنُّونَ ⑪

وَإِذَا شَأْنُهُ عَلَيْهِمْ أَتَيْنَا بَيِّنَاتٍ مَّا كَانَ حُجَّتُهُمْ إِلَّا أَن قَالُوا اسْتَوَىٰ بَابُنَا إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ⑫

قُلِ اللَّهُ يُعَذِّبُكُمْ ثُمَّ يُبَيِّنُكُمْ ثُمَّ يُجْزِيكُمْ ۚ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ⑬

27. Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. Na siku kitakapotokea Kiama, siku hiyo wataangamia wanaokamatana na batili.

28. Na utauona kila uma umepiga magoti (siku hiyo); na kila uma utaitwa kwenda (kusoma) kitabu chao (waambiwe) "Leo mtalipwa yale mliyokuwa mkiyatenda."

29. "Hili daftari letu linakwambieni kweli: bila shaka tulikuwa tukiyaandika yale mliyokuwa mkiyatenda."

30. Ama wale walioamini na wakatenda mema, Mola wao atawaingiza katika rehema yake; huku ndiko kufanikiwa kuliko dhahiri.

31. Na wale waliokufuru (wataambiwa): "Je! Hazikuwa Aya zangu zikisomwa kwenu; nanyi mkajivuna na mkawa watu waovu?"

32. Na inaposemwa: "Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli na Kiama hakina shaka, mlikuwa mkisema: "Hatujui Kiama ni nini; hatudhani ila dhana tupu wala hatuna yakini."

33. Basi ubaya wa waliyoyatenda utawadhihirikia na yatawazunguka yale waliyoyafanyia mzaha.

34. Na itasemwa: "Leo tunakusahauni (Motoni) kama nyinyi mliyosahau siku yenu hii; na mahali penu ni Motoni, wala hamna wa kukunusuruni."

وَلِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَيَوْمَ تَقُومُ
السَّاعَةُ يُحْشَرُ الْمَبْطُلُوْنَ ۝

وَتَرٰى كُلَّ اُمَّةٍ جٰثِيَةً كُلُّ اُمَّةٍ تُدْعٰى
اِلٰى كِتٰبِهَا الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ۝

هٰذَا كِتٰبُنَا يُنْفِثُ عَلَيْكُمْ بِالْحَقِّ ؕ اِنْ
كُنَّا نَسْتَنۡسِخُ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ۝

فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
فَبَدِّلْ خُلُوفَ رُبُّهُمْ فِيْ رَحْمَتِهٖ ذٰلِكَ هُوَ
الْقَوْدِ الْيُسۡبِيۡ ۝

وَ اَمَّا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا اَقَلَمَ سَكَنَ اِلٰيَّ تَنْتَلٰى
عَلَيْكُمْ فَاَسْتَكْبَرْتُمْ وَكُنْتُمْ قَوْمًا مُّجْرِمِيۡنَ ۝
وَ اِذَا قِيلَ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّ السَّاعَةُ
لَا رَيْبَ فِيْهَا قُلْتُمْ لَمَّا نَذَرۡنَا مَا السَّاعَةُ
اِنْ نَّظُنُّ اِلَّا ظَنًّا وَّمَا نَحْنُ بِمُتَّقِيۡنَ ۝
وَبَدِّلَ اللّٰهُ سَبِيۡلَاتِ مَا عَمِلُوْا وَحَاقَ بِهٖمْ مَا
كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهۡزِءُوْنَ ۝

وَقِيلَ الْيَوْمَ نَنْسِفُكُمْ كَمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ
هٰذَا وَمَا وَاوَكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمۡ مِّنۡ نّٰصِرِيۡنَ ۝

mzima, kama ilivyo katika Aya ya 53 ya Surat Fussilat inayosema, "Tutawaonyesha (ukweli wa) maneno yetu Ulimwengu mzima na kwa nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kuwa (hii dini ya Uislamu) ni HAKI".

Na lililotokea 20th July, 1969 ni kupata uwezo bin-adamu kufika kwenye mwezi akaukanyaga mchanga wake kwa mguu wake; baada ya kuondoka hapa ardhi mwezi 16th July, 1969 wakarejea mwezi 24 July, 1969. 16th July, 1969 ulikuwa Jumaatano mwezi mosi mfunguo Nane 1389.

Na Mwenyezi Mungu kayasema haya katika Aya ya 13 ya Suratul JATHIYA na Aya ya 20 ya Surrat Luqman na Aya nyinginezo. Kasema "Amekudhalilishieni vilivyoko kwenye ardhi na vilivyoko mbinguni."

Basi ukweli wa Uislamu unazidi kuonekana. Alhamdulillah.

Na kabla ya kufika hawa waliotika nalijibu Mombasa — yapata miaka 15 hivi — kuwa itamkinika kufika kwenye mwezi. Na ikatoka jawabu yetu hii magazetini. Aliitangaza Professor Ali Al-Amin. Bahati mbaya sina nakala yake. Na mara nyingi nikayasema maneno haya kwenye Radio na kwenye darasa zangu za Unguja na Mombasa na kwengineko.

17. Hapana kitu kibaya kama hasadi. Anaikataa mtu haki vivi hivi kinagaubaga, akakhitari kutiwa Motoni kuliko kulifuata la haki, kwa kuwa limesemwa na adui yake. Wakasema katika ukatiri wao: *An Nar Walal Aar*, yaani kheri Moto wa Jahanamu kuliko aibu ya Duniani! Wanasalimiwa na bwana wa kweli wa Kiislamu — Sayyidnal Hasan bin Ali bin Abi Talib — aliyesema kinyume cha haya kuwa: *Al Aar Khayrum Minan Nar*, yaani bora aibu ya dunia kuliko Moto wa Akhera.

21. Wasijidanganye bure waovu wakajitia pambani kuwa watapata siku ya Kiama watakayoyapata watu wema. Ameyapinga Mwenyezi Mungu haya mahala pengi katika Qurani kama Aya hii na ya 35 ya *Suratul Qalam* na nyinginezo.

35. "Hayo (yaliyokupateni) ni kwa sababu nyinyi mlizifanyia mzaha Aya za Mwenyezi Mungu; na maisha ya dunia yakakudanganyeni." Basi leo hawatatolewa humo wala hawatakubaliwa udhuru wao.

36. Basi sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na Muumba wa ardhi, Muumba wa walimwengu wote.

37. Na ukubwa ni wake mbinguni na ardhini, Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

ذِكْرُكُمْ يَأْتِيكُمْ التَّغْدَتُمْ أَيْتَ اللَّهِ هُزُوا
وَعَرَّتْكُمْ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فَالْيَوْمَ لَا
يُخْرِجُونَ مِنْهَا وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ۝

قُلِ لِلَّهِ الْحَمْدُ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَرَبِّ الْأَرْضِ رَبِّ
الْعَالَمِينَ ۝

وَلَهُ الْكِبَرِيَاءُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝



Ina Aya 35

SURATUL AHQAF (Imeteremka Makka)

Ina Makara 4

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Haa Mym.

2. Uteremsho wa Kitabu (hiki) umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, (na) Mwenye hikima.

3. Hatukuziumba mbingu na ardhi wala yaliyomo baina yake ila kwa haki na kwa muda uliowekwa; na wale wanaokufuru wanayapuuza (maonyo) wanayoonywa.

4. Sema: "Je! Mnaonaje wale mnaowaabudu mkamwacha Mwenyezi Mungu?" Nionyeshehi kipi walichokiumba katika ardhi, au wanayoshirika katika mbingu? Niteeni Kitabu kilichokuwa kabla ya hiki au alama yoyote ya ilimu (ya kuthubutisha haya mnaoyasema); ikiwa mnasema kweli.

5. Na wapotofu (wapotevu) wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu ambao hawatawajibu mpaka siku ya Kiama, na hawatambui dua zao.

6. Na (ambao) watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.

7. Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale waliokufuru husema juu ya haki inapowajia: "Huu ni uchawi ulio dhahiri."

8. Au wanasema: "Ameyatunga, (ameyabuni ameyazua) mwenyewe." Sema: "Ikiwa nimeyatunga mimi, basi hamuwezi kunifaa chochote mbele ya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمْدٌ

تَنْزِيلٍ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ①

مَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى، وَالَّذِينَ كَفَرُوا عَمَّا أُنذِرُوا مُّعْرِضُونَ ②

قُلْ أَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ، إِيْتُونِي بِكِتَابٍ مِّمَّنْ قَبْلَ هَذَا أَوْ أَنزِلْهُ مِنْ عِلْمٍ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ③

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّنْ يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنْ دُعَائِهِمْ غَفُولُونَ ④

وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ⑤

وَإِذَا نُتِلَتْ عَلَيْهِمْ أَنْبَاءُ بَيْنَتِ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَنَا جَاءَهُمْ هَذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ⑥

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ، قُلْ إِنْ افْتَرَيْتُهُ فَلَا تَمْلِكُونَ لِي مِنَ اللَّهِ شَيْئًا، هُوَ أَعْلَمُ بِمَا

4. Makadiyani wamepachikia katika hii Aya waliyoifanya ya 5 maneno haya:— "Hao wanaosadiki ya kuwa Nabii Isa alipata kuumba vitu, sasa watokee kujibu hoja hii ya Mwenyezi Mungu . . ." Wametia haya ili kupinga ile miujiza ya Nabii Isa aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Na moja katika hiyo ni kufanya ndege wa udongo wakaruka, kisha wakaanguka wakafa. Sisi tunamsadiki Mwenyezi Mungu alivyosema kama tulivyobainisha haya katika marejezo ya Aya ya 49 ya Surat Aali Imran. Wao wanamkanusha Mwenyezi Mungu — khiyari yao.

5-6. Mara nyingi zimekuja simango hizi za kusimwangwa wanaowaomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu.